

More past papers are available on <http://www.kenyaplex.com>

KCSE Kiswahili Revision Past Paper

PARKLANDS BOYS" HIGH SCHOOL
MAZOEZI YA MARUDIO.

1. Andika ngeli za nomino hizi:-

- a. Bustani
- b. Glasi
- c. Ndimi
- d. Dagaa
- e. Manukato
- f. Kipeo

2. Tunga sentensi ukitumia nomino ya ngeli ya I-I pamoja na kionyeshi cha mbali.

3. Tumia shina la kimilikishi cha nafsi ya tatu wingi pamoja na ngeli ya LI-YA kutunga sentensi.

4. Andika sentensi zifuatazo katika hali ya wingi.

- a. Ua unaozunguka uwanja wa ndege ni madhubuti.
- b. Asali tamu ni ile haijaongezwa kemikali.
- c. Kucheza kunakofurahisha ni kwake.
- d. Upana huu unafaa kwa ujenzi wa nyumba ile.

5. Taja sifa bainifu za:

- a. /u/ /e/
- b. /j/ /ch/

6. Linganisha sauti hizi mbili (l) na (r) ukirejelea

- i. Mahali pa kutamkia
- ii. Jinsi ya kutamka

7. Taja sauti mbilimbili ambazo ni:

- a. Vipasuo
- b. Nazali
- c. Vikwamizo

8. Eleza tofauti baina ya irabu na konsonanti.

9. Taja matumizi ya (,) kama kiakifishi na kwa kila matumizi uonyeshe mfano.

10. Tumia alama zifuatazo katika sentensi:

- a. ;
- b. /

11. Akifisha sentensi zifuatazo:

- a. Maskini mtoto yule atagongwa na gari
- b. Ni lini utajifunza kuheshimu watu.

12. Tambulisha aina za maneno yaliyotumiwa katika sentensi zifuatazo:

- a. Jamani! Msaidieni ajuza huyo.
- b. Jana jioni waliburudishwa baada ya chajio.
- c. Matunda haya na yale mabivu yatauzwa.

13. Onyesha viambishi awali na tamati katika:

- a. Watatukaribisha
- b. Vilinunuliwaje?
- c. Wamewasameheha.
- d. Uliotatizika.